SURA YA TISA

MUDA

“ Muda ulikuwepo, muda upo, muda hautakuwepo zaidi”, W.Marsdori anasema.

“Muda unapimwa vizuri na machozi” A.J Raya, Hazina zote za dunia haziwezi kurudisha muda uliopotea”, mtu Fulani alisema “ huwa hatujali muda ila kutokana na hasara yake”, Young

Mwanafunzi ni bundi ufahamu kuwa muda kwako ni hazina ya pekee na muhimu sana kwako.Sababu ambazo zinanifanya niseme hivi ni hizi zifuatazo kwako mwanafunzi kila kitu kimepangika katika muda ,Angalia vipindi vimepangwa kwa dakika arubaini ,masomo yamepangwa kimuhula,mitihani ,majaribio , vimewekewa muda na hatimaye kidato chenyewe kimepangiwa muda wa mwaka mmoja.

Hii ina maana kuwa mwanafunzi huna muda wa kupoteza kwa kitu chochote ambacho hakikusaidii katika masomo yako lazima awe makini na muda , wanafunzi wa karne ya ishirini na moja wanapata shida sana kuchagua elimu kama kipaumbele wakati huu.Muda huu anataka agawe kwa vitu vingine kama kuingia mtandaoni bila sababu ya kishule au kimasomo,Anataka ashangilie mpira unaochezwa ulaya au kwingineko popote duniani , anataka aangalie tamthilia au movies , anataka aangalie wanamuziki, anataka asikilize muziki na achezee simu. Wanafunzi watakao kuwa hodari kukataa kuchukuliwa muda wao na mambo hayo ndio watakao kuwa washindi ,tatizo ni muda gani vitu hivyo vitatumia katika muda wako wa ziada, ambao unaumiliki kama huwezi kupanga muda kwa ajili ya masomo yako basi wewe unapanga kushindwa kimasomo .Ni juu yako kupanga ratiba ya masomo na kuifuata.

Charles Darwin alisema na hapa nanukuu “ **Mtu ambaye anapoteza saa moja hajui thamani ya maisha”** mwisho wa nukuu.Kama unapoteza muda hovyo hovyo wakati wewe ni mwanafunzi ni ishara kuwa huna malengo yoyote na shule.Maisha yanamtaka mwanafunzi makini anayejua kipaumbele chake kwa sasa ,kumbuka muda ulionao ni wa shule tu,Vitu vingine si vipaumbele achana navyo.Tumia muda kadri unavyoweza kwa ajili ya masomo yako .Ni shule ambayo itakuja kukubadisha majina kutoka bwana ,mpaka,muheshimiwa Daktari na hata profesa. Unaonaje majina yanavyozidi kupanda ndivyo yanavyozidi kukupendeza na kuwa mazito na matamu kusikika masikioni mwa watu.

Kumbuka sana maneno ya Swami Vivekemanda ambavyo alisema na hapa namnukuu " **Chukua wazo moja lifanye kuwa maisha yako , liote lifikirie liishi, hakikisha viungo vyako vyote vimejaa wazo hilo, mishipa , misuli, ubongo,Halafu funga mlango wazo lingine lisiingie hii ndiyo siri ya mafanikio**" mwisho wa nukuu. Muda wako wa shule ni mdogo sana na hivyo usiingize mambo mengine katika ratiba ya masomo .Michelongelo anasema na hapa namnukuu " **hakuna madhara ambayo yanazidi yale ya kupoteza muda ".**

Pamoja na ratiba ya darasani ni muhimu mwanafunzi kujipangia ratiba ya kujisomea kama mwalimu hayupo darasani ,Ni pamoja na unaporundi nyumbani kumbuka ili uwe mashuhuri lazima ujishinde mwenyewe lazima uzidishe bidii ya kujisomea .Erick Thomas anasema na hapa namnukuu " **wewe unataka kufanikiwa vibaya kiasi gani ?"** mwisho wa nukuu .Wewe una njaa kiasi gani na mafanikio katika elimu.

Kama ukitumia vizuri muda wako bila kujidanganya basi lazima utabadilisha matokeo ya mitihani. Epuka kusoma na huku unaangalia Tv au unasikiliza nyimbo. Akili yako ina uwezo wa kushika kitu kimoja kimoja tu. Kumbuka muda ni mali na muda ni mama wa mafanikio yote. Muda utaenda bure bila wewe kuelewa ipasavyo unachosoma. Kila unachofanya jiulize, je ninakuwa bora katika masomo ninapofanya jambo hili? Peter Drucker anasema, "**Hakuna kitu kisichokuwa na maana kama kufanya kitu kwa ustadi kitu ambacho hakistahili kufanywa kabisa**."

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb. Na. PY/BC. 40/265/01/80

Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
Jengo Na. 10,
S. L. P. 10,
40479 DODOMA.

Tarehe: 31/08/2017

Bw. Ptrick Y. Sikayinda,
S.L.P 9560,
DAR ES SALAAM.

YAH : KITABU CHA "ZIJUE SIRI ZA KUFANIKIWA KATIKA MASOMO"

Rejea barua yako ya tarehe 07/08/2017 tuliyoipokea tarehe 15/08/2017 kuhusu mada tajwa. Napenda kukufahamisha kwamba tumepitia maudhui ya kitabu chako kama ulivyoomba na kubaini kuwa ni kitabu kilichochoheni mikakati ya mabadiliko ya tabia na mienendo ya wanafunzi na vijana kwa ujumla ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa inachangia kutofanya vizuri katika mitihani yao. Kitabu chako kimeainisha vyanzo mbalimbali vinavyochangia matokeo mabaya katika masomo na maisha kwa ujumla. Kitabu hiki kinawafaa pia walimu pamoja na wazazi au walezi katika malezi ya vijana hususan katika kipindi hiki chenye mmomonyoko mkubwa wa maadili miongoni mwa jamii.

Kwa ujumla ni kitabu ambacho kinaweza kutumika shuleni kama Kitabu cha Ziada (Supplementary book). Hata hivyo, kitabu chako kitaweza kutumika katika shule za sekondari iwapo utakiwasilisha Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili wataalam wakipitie kwa kuzingatia vigezo vya kiuandishi vilivyowekwa na iwapo kitakidhi vigezo na kuidhinishwa kitaweza kutumika. Hivyo, nakushauri uwasiliane na Taasisi ya Elimu Tanzania ili wakupatie maelekezo ya jinsi ya kuwasilisha nakala za kitabu chako kwa ajili ya uchambuzi.

Dkt. Ave Maria Semakafu
Kny: KATIBU MKUU

Nakala: Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),
S.L.P 35064,
DAR-ES-SALAAM.